

RIWAYA YA KISWAHILI: JICHO FICHUZI NA ANGAZI LA VIVUTIO VYA UTALII ZANZIBAR

Masoud Nassor Mohammed & Geoffrey Kitula King’ei

Ikisiri

Lugha ya Kiswahili na fasihi yake zinajengana. Kukua kwa lugha ya Kiswahili kunaimarisha ukuaji wa fasihi ya Kiswahili. Kwa upande mwingine, kukua kwa fasihi ya Kiswahili kunaimarisha pia maendeleo ya lugha ya Kiswahili. Kwa pamoja, maendeleo ya lugha ya Kiswahili na fasihi yake yanachangia kwa kiasi kikubwa kuimarika kwa sekta ya utalii ambayo inachangia kukua kwa uchumi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Fasihi ya Kiswahili, hasa riwaya, ina mchango mkubwa katika kuvifichua, kuvionesha, kuvitangaza na kuvieleza vivutio vya utalii katika visiwa vya Zanzibar. Hatimaye, watalii wa ndani na nje ya nchi, hutembelea na kuchangia pato la taifa na la watu binafsi. Makala inaangalia namna baadhi ya riwaya za Kiswahili za Zanzibar zilivyoibua na kuvitangaza vivutio vya utalii visiwani Zanzibar na hatimaye kuimarika kwa uchumi wake. Data za makala imekusanywa kwa njia ya udurusu wa matini za riwaya teule nne: Kiu (1972), Asali chungu (1977), Vuta n’kuvute (1999), na Kosa la bwana Msa (1984). Nadharia ya uhalisia imetumiwa kuongoza uchambuzi wa data katika makala hii. Makala inatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika fasihi ya Kiswahili na uimarishaji wa sekta ya utalii Afrika ya Mashariki hasa katika kipindi hiki cha hamasa ya uchumi wa buluu Zanzibar.

Utangulizi

Itakumbukwa kwamba katika miaka ya hivi karibuni nchi nyingi duniani zimeingia katika uwekezaji wa sekta ya uchumi wa buluu (uchumi unaohusiana na bahari). Zanzibar ikiwa ni mojawapo ya maeneo ya dunia imejibainisha na kujielekeza zaidi katika eneo hilo (Ilani ya CCM, 2020-2025:188). Rais wa awamu ya nane wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar amekuwa mstari wa mbele katika kupigania sekta hiyo. Mikakati na juhudi kadhaa zinafanywa ili kufikia azma hiyo. Mfano mmojawapo ni uundwaji wa wizara maalumu ya uchumi wa buluu katika serikali ya awamu ya nane. Sekta ya utalii hasa ule unaohusiana na bahari ni kipengele muhimu cha uchumi wa buluu. Mbali na utalii wa bahari, upo utalii wa aina nyingine mbalimbali unaohamasishwa kwa ajili ya kukuza uchumi wa Zanzibar. Waandishi wa riwaya nao wana mchango katika kuisaidia serikali kupanga na kutekeleza mikakati ya kimaendeleo. Hivyo, nao

wamebainisha na kuvitangaza vivutio mbalimbali vya utalii Zanzibar. Kwa kufanya hivyo, wamesaidia kuwavutia watalii wa ndani na nje ya Zanzibar kuyatembelea na kuchangia pato la taifa na maendeleo yake. Kuangalia jambo hili, waandishi wa makala wamechunguza riwaya teule za Kiswahili za waandishi wa Zanzibar na kuonesha namna walivyobainisha maeneo ya kitalii visiwani humo.

Katika kufanya hivyo, watafiti walijikita katika kuangalia vivutio vya kijiografia, kiutamduni na kihistoria vilivyobainishwa na waandishi hao. Riwaya zilizopitiwa ni *Kiu* (1972) ya mwandishi Mohammed Suleiman; *Asali chungu* (1977) ya Said Ahmed Mohammed; *Vuta n'kuvute* (1999) ya Shafi Adam Shafi; na *Kosa la bwana Msa* (1984) ya mwandishi Mohammed Said Abdulla.

Maelezo mafupi kuhusu waandishi na riwaya teule

Katika sehemu hii, makala imetoa maelezo mafupi kuwahusu waandishi wa riwaya nne zilizoteuliwa na kuchunguzwa katika utafiti huu. Maelezo mafupi kuzihusu riwaya zenyewe pia yamewekwa kwa lengo la kuzitambulisha.

Waandishi wa riwaya teule

Waandishi wa riwaya zilizoteuliwa kufanyiwa utafiti huu ni maarufu na weledi katika fani ya uandishi wa riwaya. Mohammed Suleiman Mohamed ambaye ameandika riwaya ya *Kiu* na *Nyota ya Rehema* amepata umaarufu mkubwa ndani na nje ya Zanzibar. Riwaya zake zinasomwa na kutahiniwa katika mitaala mbalimbali ya elimu. Aidha, kutokana na riwaya zake hizo amewahi kupata tunzo mbalimbali za uandishi bora. Kwa mujibu wa Bertoncini (1965), Mohamed Suleiman anatambulika nchini mwake kama mtunzi hodari zaidi wa riwaya ya Kiswahili. Mbatia (2016) anasisitiza kuwa kama Kezilahabi alivyowakilisha kilele cha upevu wa riwaya Tanzania bara ndivyo Mohamed Suleiman alivyowakilisha kilele hicho visiwani Zanzibar. Mohamed Suleiman amezaliwa Koani, Wilaya ya Kati, kisiwani Unguja mwaka 1943.

Naye Said Ahmed Mohammed Khamis ni mwandishi nguli wa tanzu zote za fasihi andishi; ameshaandika vitabu zaidi ya 60 hadi sasa (Mohammed, 2017). *Asali chungu* ni riwaya

yake ya kwanza aliyoiandika mwaka 1977. Baada ya riwaya hiyo ameandika riwaya nyingine kadhaa zikiwamo *Utengano* (1980), *Dunia yao* (2006), *Kamwe si mbali tena* (2014) na *Nyuso za mwanamke* (2010). Mbali na riwaya, anazo pia tamthiliya, mashairi na hadithi fupi kama vile *Kivuli kinaishi* (1990), *Amezidi* (1995), *Kiti cha moyoni katika mkusanyo wa kiti cha moyoni na hadithi nyingine* (2007), *Kina cha maisha* (1984) na *Sikate tamaa* (1982). Said Ahmed alizaliwa Wete, kisiwani Pemba mwaka 1947. Kwa sasa ni Profesa mstaafu katika taaluma za fasihi ya Kiswahili.

Kwa upande mwingine, Shafi Adam Shafi ni mwandishi hodari wa riwaya ya Kiswahili. Riwaya yake ya *Vuta n'kuvute* (1999) imekuwa ikitumiwa kwa miaka mingi katika mitaala ya elimu ya sekondari Tanzania. Ameandika pia riwaya nyingine kama vile: *Kuli* (1979) na *Mbali na nyumbani* (2013), *Mtoto wa mama* (2018). Shafi Adam amezaliwa mwaka 1940 Mjini Zanzibar.

Mwishoni ni Mohamed Said Abdullah, almaarufu Bwana Msa. Mwandishi huyu mkongwe wa riwaya anatajwa kuwa mwandishi wa kwanza aliyeandika riwaya ya Kiswahili yenye sifa kamili za riwaya. Alianza kuandika riwaya tangu mwanzoni mwa miaka ya 1960. Miongoni mwa riwaya zake maarufu ni *Kosa la bwana Msa* (1984), *Mzimu wa watu wa kale* (1960), *Kisima cha giningi* (1968), *Siri ya sifuri* (1974), na *Mwana wa yungi hulewa* (1976). Alizaliwa Zanzibar mwaka 1918 na alifariki mwaka 1992.

Maelezo mafupi kuhusu riwaya teule

Katika utafiti huu, riwaya nne za waandishi waliodokezwa hapo juu ziliteuliwa. Riwaya zilizoteuliwa ni *Vuta n'kuvute*, *Asali chungu*, *Kosa la bwana Msa* na *Kiu*. Riwaya hizi zimeandikwa kuakisi mandhari ya Zanzibar katika nyakati tofauti. Kwa namna ya kipekee, kazi husika zimeuakisi vizuri utamaduni wa Wazanzibari. Zimeyasawiri vyema maisha ya watu wa visiwani na harakati zao hasa za kujinasua kutoka katika ukoloni.

Tukianza na riwaya ya **Asali chungu**, ni miongoni mwa kazi za sanaa kutoka visiwani Zanzibar. Riwaya hii inayamulika maisha ya jumla katika kipindi cha utawala wa kikoloni. Mwandishi ametumia migogoro katika familia ya bwana Zubeir kuwakilisha hali ya maisha

katika jamii kwa wakati huo. Bwana Zubeir ni Mkuu wa Wilaya (DC) katika utawala wa wakati huo. Bi. Amina ni mkewe aliye na uwezo kiuchumi. Ana pesa anazozitumia kuwateka vijana. Bwana Zubeir anawanyanyasa wananchi kwa njia mbalimbali. Anaowadhulumu zaidi ni wanawake. Anawalazimisha wasichana warembo kushirikiana naye kingono. Bwana Zubeir anambaka Semeni ambaye ni mtumishi wake. Kitendo hiki kinayaharibu maisha ya Semeni. Baada ya kubakwa, Semeni anakuwa kahaba. Bi. Amina kwa upande wake, hatoshelezwi kimapenzi na mumewe, bwana Zubeir. Anawanasa vijana wadogo kama vile Dude na kuwatumia katika kuzima uchu wake. Katika njama zake, anawatumia Bushiri na Biti Daudi ambaye pia bwana Zubeir anatumia kwa njama kama hizo. Amina anatamani mumewe afe ili waweze kuishi na Dude kama mume na mke. Baada ya Dude kukosana na Bi. Amina na kuhama, anarudiana baadaye na Shemsa, binti yake Bi. Amina, kama mchumba wake na hatimaye wanaoana. Muda mfupi kabla Bi. Pili kufariki, anamdokeza Dude kwamba bwana Zubeir ndiye babake. Ikumbukwe kuwa, Dude alizaliwa baada ya bwana Zubeir kumbaka Semeni. Dude anajua jambo hili baada ya kushirikiana kimapenzi na Bi. Amina ambaye ni kama mama yake wa kambo; Shemsa na Latifa ambao ni dada zake. Baada ya kifo cha bwana Zubeir na Bi. Amina, Dude, Shemsa na Latifa wanashikana mikono.

Kwa upande mwingine, riwaya ya *Kiu* iliyoandikwa na Mohamed Suleiman imeegemezwa katika dhamira kuu ya tamaa. Tamaa za aina mbalimbali zimewasilishwa pamoja na madhara yake. Riwaya imeanza kumuonesha bwana Mwinyi mwenye umri usiopungua miaka sitini akiwa na utajiri mkubwa wa mali. Mwandishi anatuonesha kuwa Mwinyi alikuwa na uwezo wa kununua chochote ambacho angekitamani. Hata hivyo, utajiri wote alionao uliingia kasoro kutokana na kukosa kitu kimoja tu, ambacho hakuweza kukinunua kwa fedha zake. Ilikuwa ni hiari ya mtu mwingine. Hiyari ya Bahati. Bahati, msichana mdogo wa umri, alibahatika kuonana na bwana Mwinyi. Tangu siku aliyomuona, Mwinyi alichanganyikiwa naye, alijenga tamaa kubwa ya kimapenzi. Tamaa hii ilimfanya awe tayari kupoteza chochote kama si vyote alivyonavyo ili ampate Bahati. Alimshirikisha Idi, dereva wake ili kufanikisha mpango wa kumpata Bahati.

Idi naye aliitumia fursa hiyo kumlaghai na kukidhi tamaa yake ya kifedha. Alimshawishi Bahati washirikiane kumuibia Mwinyi. Bahati kwa shingo upande, na baada ya kutishiwa kuwa iwapo hatakubali hatakuwa naye kimapenzi, anakubali kushiriki katika utapeli huo. Wanafanikiwa kumuibia kiasi kikubwa cha fedha ambacho kinawawezesha kuanzisha maisha yao na kujenga nyumba yao ya kifahari huku wakimtia tamaa Mwinyi juu ya kumpata Bahati. Walipotosheka na fedha walizomuibia walimkimbia. Walimuacha Mwinyi akiwa katika hali mbaya ya kiafya iliyozoroteshwa zaidi na tamaa ya kimapenzi. Idi anamuoa Bahati na wanaishi raha mustarehe kwa muda mchache tu katika nyumba yao waliyojenga. Baada ya muda huo mchache Idi anambadilikia Bahati na kumgeuka. Anamdharau na kutomthamini tena. Idi anakuwa mlevi, mzinzi na jeuri mkubwa kwa mkewe. Anadiriki kuleta wanawake mpaka ndani ya nyumba yao. Bahati anapogundua hilo, na kumuonya mumewe, Idi anamwacha na kumfukuza bila chochote.

Bahati anarudi kwao huku akiwa na kilio kilichochanganyika na majuto. Baada ya kupewa ushauri na kutafakari, Bahati anaamua kumwandikia Idi barua ya kudai haki yake na kumuonya kuwa iwapo hatampa haki yake atamfikisha katika vyombo vya sheria. Alipopokea barua hiyo, Idi anarudisha majibu kuwa hana nia ya kumdhulumu mali yake na kwamba yupo tayari kumpa sehemu ya mali waliyochuma pamoja. Katika barua ya majibu, Idi anamuelekeza Bahati wakutane ili kuzungumzia jambo hilo kwa kina zaidi.

Bahati anajiandaa kwa furaha kubwa kwenda kuonana na Idi katika miadi yao jioni waliyokubaliana. Bahati alitoka kuelekea sehemu ya miadi yao. Muda ulianza kuhesabu saa moja, ya pili, ya tatu na kuendelea. Bahati hakurudi tena na hakuonekana tena mpaka leo hii.

Nayo riwaya ya *Kosa la bwana Msa* inayaangazia maisha halisi ya Zanzibar. Inamsawiri bwana Sayyid Ahmed bin Soud, tajiri mwenye sharafu kubwa visiwani Zanzibar zama hizo. Ahmed bin Soud bila kumuarifu mke wake Bi. Shinuna, anaoa mke mwingine na kumhifadhi Chwaka - Mkoa wa Kusini Unguja. Anamuaga mke wake wa kwanza kusafiri ilhali anaishia Chwaka kwa mke mdogo. Mke mkubwa anapogundua anapanga njama ya kumuua kwa kuwatumia vijana wahalifu. Hali hiyo inamfanya Jamila, mke mdogo kuondoka nyumbani kwake kwa lengo la kumsitiri aibu mume wake. Hii ni kutokana na hadhi aliyonayo. Anakimbilia

kwa Mwanatenga na hatimaye kuolewa Arabuni. Mume wake anafariki katika ajali huku akimwachia Jamila, mtoto mmoja. Inabainika baadaye kwamba bwana Sayyid Ahmed alimuoa Jamila kwa jina tofauti. Huko alitumia jina la Ali bin Soud. Kwa sababu hiyo, ndipo bwana Msa alichukua maamuzi ya kumuoza mume mwingine huko Arabuni kwa madai kuwa ndoa ya awali haikuwa sahihi. Hapo ndipo panakuwa chanzo cha kosa la bwana Msa. Baadaye, bwana Msa anakiri kosa hilo na kuwaomba radhi wahusika wote.

Mwishoni kabisa, riwaya ya *Vuta n'kute* ya Shafi Adam Shafi. Katika riwaya hii, Shafi anazungumzia vuguvugu la kudai uhuru wa Zanzibar. Katika jambo hilo kunaibuka mivutano mikubwa baina ya jamii na utawala uliokuwapo; na mvutano baina ya tamaduni mbalimbali zilizounda jamii ya Zanzibar. Kwa mfano, Yasmin, mtoto wa Kihindi analazimishwa na wazazi wake kuolewa na bwana Raza, mzee sawa na babu yake. Yasmin anaamua kumtoroka na kurudi nyumbani kwao. Yasmin anafukuzwa na wazee wake kwa kumwacha Raza. Katika upweke wake anasitiriwa na Mwajuma, shoga yake anayeishi maisha ya starehe mjini. Yasmin anaingizwa uswahilini na anakuwa sehemu ya maisha ya shoga yake, Mwajuma. Baadaye Yasmin anaolewa na Shihab lakini mume huyo anafariki kwa wivu. Yasmin anampenda sana Denge, kijana wa Kiswahili anayeongoza mapambano ya kudai uhuru. Hata hivyo, Denge anakosa muda wa kushughulika na Yasmin. Kwake yeye, maisha ni mapambano dhidi ya ukoloni tu. Mvutano unakuwa mkali na hatimaye Denge anaamua kutoroka nchi. Ingawa anaondoka lakini anasisitiza kuwa hii ni Vutu n'kuvute ambayo sharti yeye Denge na wenzake washinde.

Nadharia iliyotumika

Makala iliongozwa na nadharia ya uhalisia. Msokile (1993) anaueleza uhalisia kama mtindo wa sanaa wa kuonesha maisha kama yalivyo. Anaeleza kuwa uhalisia ulianza mwaka wa 1820 B.K. Msingi wa nadharia hii ni kuwa sanaa inatarajiwa iseme ukweli, iwe aminifu na ioneshe hali halisi ya mazingira. Njogu & Chimera (1999) wanadai kuwa katika fasihi ya Kiswahili, tapo la uhalisia lilizuka baada ya mwaka 1970. Senkoro (1998) anadai kuwa nguvu mbalimbali za kijamii zilichangia kuzuka kwa uhalisia katika fasihi ya Kiswahili. Nguvu hizo za kijamii kwa

mujibu wa Senkoro (keshatajwa) ni: ukoloni mamboleo, Azimio la Arusha, Mapinduzi ya Zanzibar, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na Ujamaa vijijini. Hii ina maana kwamba kazi nyingi zilizoandikwa kwa kuegemea katika mkabala wa uhalisia zinafanikisha kudhihirisha uhistoria kutokana na kujiegemeza katika matukio halisi ya kihistoria.

Mbatia (2001) anafafanua uhalisia kama istilahi inayorejelea kimsingi mtindo wa uandishi unaojishughulisha na utoaji wa taswira halisi ya maisha ya kawaida katika jamii mahususi. Kutokana na maelezo haya, tunaona kuwa nadharia ya uhalisia hujikita katika ukweli wa hali halisi ya maisha katika jamii mahususi. Kwa mnasaba wa tapo hili la nadharia, waandishi wa makala hii walichunguza riwaya teule na kubainisha mambo halisi yaliyosawiriwa katika riwaya hizo ambayo ama ni ya kihistoria, kijiografia au ya kiutamaduni katika visiwa vya Zanzibar. Mambo hayo yanabainiswa katika sehemu inayofuata hapo chini.

Mchango wa riwaya katika kufichua na kutangaza vivutio vya utalii

Katika sehemu hii, makala inafafanua matokeo ya utafiti. Data zilizokusanywa na kuchambuliwa kiuhalisia kutoka katika riwaya teule, zimeonesha michango anuai ya waandishi wa riwaya hizo katika kusaidia kuvifichua na kuvitangaza vivutio vya utalii. Kila riwaya kwa namna yake imejaribu kuyafikia maeneo ya kijiografia, kihistoria na kiutamaduni yanayogusa moja kwa moja sekta ya utalii katika visiwa vya Zanzibar. Ingawa riwaya zimegusia mambo mengi, hapa tulijaribu kuyaangalia machache kwa muktadha wa makala hii ambapo tulielezea kuhusu fukwe za bahari, magofu ya kihistoria, Bei el Ajab na Mji Mkongwe, Mwaka Kogwa, eneo la Darajani, mabaki ya kikoloni na utamaduni wa taarab.

Fukwe za bahari

Moja ya kivutio kikubwa cha utalii visiwani Zanzibar ni fukwe za bahari. Katika maeneo mbalimbali ya fukwe katika kisiwa cha Unguja na Pemba, kumejengwa hoteli kubwa za kifahari kwa ajili ya watalii na utalii. Katika maeneo hayo, hasa yale yenye mchanga mweupe, watalii hupendelea kukaa na kustarehe kwa namna mbalimbali. Jambo hili limedokezwa na riwaya zilizochunguzwa. Kwa mfano, katika riwaya ya *Asali chungu*, (uk. 116) mwandishi anasimulia:

Nyumba ya Bi. Amina imejengwa karibu na ufukwe nyuma ya kisiwa cha Webu, imejitenga kutafuta faragha mbali na vijumba vya kijiji chenyewe. Kwa namna ilivyosimama imependeza kwa ubetebete wake na paa lake jekundu la bati. Kwa pale kisiwani, hiyo ilikuwa nyumba pekee iliyovutia. Kwa ukubwa labda inashindana na ule Msikiti lakini kwa uzuri hapana nyingine inayoweza kuivua kilemba. Usiku kiasi cha saa tatu baada ya kwisha kunywa chai yao walijizamisha faraghani mahali ambapo si aghlabu mtu kuweza kupita ila kwa upelelezi. Walitandika kibusati ufukweni kwenye mchanga mweupe, wakalala huku wameegemeza vichwa vyao mitoni. Ulikuwa usiku wa mbaamwezi, mbingu ilikuwa safi na mchanga ukimeremeta pale ufukweni, anga lilikuwa limemwangaa na kuathiri maji na miti iliyokuwamo katika mazingira yake. Miili yote ilikuwa imepakwa fedha hata Dude na Amina wakawa wamebadilika sura.

Kwa upande mwingine, naye mwandishi wa *Kiu* amegusia nafasi ya ufukwe katika masuala ya utalii kwa kusimulia:

Ilikuwa ni siku ya maji makuu, mawimbi yakinyanyuka na kujibwaga karibu na miguu ya mashoga wawili waliokuwa wakitembea. **Ufuko wote** ulikuwa umeshaliwa na maji isipokuwa ukanda mwembamba wa sehemu ya juu iliyokuwa na taka za **pwani**. Pale walipokuwapo ni kati ya ghuba. Mbele yao ufuko ulifanya upinde uliokatika vyema ukatambaa maili tatu hivi hadi kwenye rasi ya jabali lenye ncha iliyochongokea **baharini** na kwa chini likafanya mvungu mkubwa. Furaha ya watafutao faragha. Kwa pale walipokuwapo ile ncha ya jabali ilikuwa sehemu ya mwisho ya ardhi waliyoweza kuiona kupindukia pale macho hupotea katika mapovu ya mawimbi yaliyokuwa yaking'aa katika miali ya jua (*Kiu*: 129).

Madondoo haya yanaonesha namna ufukwe ulivyo na nafasi kubwa katika kuwaburudisha na kuwaliwaza watu. Ndiyo maana utalii zaidi unaonekana maeneo ya ufukweni pembezoni mwa bahari. Waandishi kuyaeleza mazingira ya ufukwe na kuusifu weupe wa mchanga wake na mandhari ya sehemu hizo ni kuutangaza utalii na kuwafanya wageni kutoka sehemu mbalimbali kufika sehemu hizo ili kujiliwaza. Fukwe ni sehemu tulivu, zenye mandhari ya kuvutia yanayotokana na mchanga wake, mawimbi ya bahari, majabali pamoja na upepo mwanana unaowafanya watu wanaofika eneo hili wajisikie raha. Haya yote yanapoelezwa na wanafasihi huwavutia watalii kuzitembelea fukwe za Zanzibar na kuinua uchumi.

Magofu ya kihistoria

Katika eneo jingine ambalo huwafanya watalii wa ndani na nje wafunge safari ni kuyatembelea maeneo ya magofu. Haya ni makaazi ya zamani ya watu. Watu hao wanaweza kuwa wa jamii ile

ile au wa kutoka ng'ambo. Kwa vyovyote vile maeneo kama Kilwa, Tumbatu, Chaani, Lushoto, Bagamoyo, Ujiji na maeneo mengine yenye nyumba za kale yamekuwa yakipokea wageni wengi kuyatazama. Kufanya hivyo nchi na wananchi wa maeneo hayo hupata kipato kinachostawisha maisha yao. Tunapoziangalia riwaya za Kiswahili za Zanzibar tunabaini kuwa hazikuacha kulisaidia taifa katika kuyataja na kuyabainisha maeneo hayo yenye magofu. Waandishi walipofanya hivyo bila shaka wamechangia pakubwa kuwavutia wageni kutoka kokote ulimwenguni kuyatembelea maeneo hayo na kukuza uchumi wa Zanzibar kutokana na fedha wanazolipa wageni hao. Tuangalie mfano ufuatao kutoka mojawapo ya riwaya zilizochunguzwa:

Usoni pale palikuwa na mteremko mrefu uliojaaliwa minazi iliyojiotea ovyo ambayo ilienea hadi ufukoni. Upepo uliokuwa ukiwafikia ulikuwa na harufu ya chumvi. Na walipotupa macho yao katikati ya minazi waliweza kuiona bahari iliyokuwa ikimeta kwenye jua la kaskazi. Kando yao palikuwa na *magofu ya majumba ya zamani* yaliyomea magugu yamesimama yakihesabu miaka. Tena upande mwingine palikuwa na miembe iliyopandwa kwa fujo labda na wale marehemu wenye magofu yale. Mahali pale palichanganya uzuri wa maumbile na ukiwa. Kwa kitambo kidogo wale vijana walisahau kitu kilichowaleta pale wakawa wanayaajabia mandhari (*Kiu: 12*).

Dondoo hili linayataja maeneo ya magofu ya nyumba kongwe ambazo zimetapakaa sehemu mbalimbali za Zanzibar kwa sababu ya historia ya ujio wa wageni. Ingawa haikubainishwa ni eneo lipi mojawapo lakini inabainishwa kuwa majengo hayo ya kihistoria yapo karibu na ufukwe wa bahari na yapo katikati ya minazi. Sehemu hiyo inaweza kuwa Maruhubi, Mtoni au sehemu nyingine yoyote inayosawirika na maelezo hayo. Mwandishi Mohamed Suleiman hapa amechangia kwa kiasi kikubwa kuvitangaza vivutio vya utalii.

Beit el Ajaib na Mji Mkongwe

Moja kati ya sehemu muhimu za kihistoria za Zanzibar ni eneo la Mji Mkongwe uliopo Zanzibar. Mji huu umeingia katika maeneo ya urithi wa dunia na unatambuliwa na Umoja wa Mataifa. Katika mji huu kuna jumba la wananchi lililopo eneo la Forodhani. Jumba hili lijulikana kama *Beit el Ajaib* (Jumba la Ajabu) lililojengwa tangu mwaka 1883 huwavutia wageni wengi. Kwa ujumla wake, eneo la Mji Mkongwe hutembelewa na watalii wengi kila mwaka na huiingizia Zanzibar fedha za kigeni pamoja na kuwapatia fursa za kitalii wenyeji wa

eneo hilo. Riwaya ya *Kosa la bwana Msa* iliyochapishwa mwaka 1984 imetaja eneo hilo na hivyo kuwa msaada mkubwa kwa wasomaji kutambua na kufika eneo hilo. Katika riwaya hiyo bwana Msa amesimulia (uk. 75):

Saa ya Beit el Ajaib iligongomea mipigo minane kwa kelele na ngurumo zake za desturi kuonesha kuwa sasa hivi itapiga majira ya saa. Wakati ulikuwa usiku na saa hiyo ilipiga mara nne. Saa nne za usiku katika nyumba moja huko Forodhani. Bi. Shinuna na mumewe Ahmed bin Soud walikuwa chumbani kwao. Chumba cha kulala. Bi. Shinuna alikuwa akibadilisha nguo zake za mchana.

Katika dondoo hili mna mambo mawili makubwa ya kuelezwa. Mosi, ni utambulisho wa jengo la Beit el Ajaib ambalo ni alama muhimu ya kuutambulisha Mji Mkongwe na Zanzibar kwa jumla. Pili, ni kuhusu saa iliyopo juu ya jengo la Beit el Ajaib. Saa hii inatajwa na mwandishi kwa namna ya kuonesha wakati na labda kuonesha hali ya kimaendeleo ya Zanzibar toka hapo kale. Ni wazi kuwa mwandishi anaonesha kuwa maendeleo ya kiteknolojia ya Zanzibar ni jambo la kitambo na linaoneshwa wazi na kuwapo kwa saa sambamba na jengo zuri la kuvutia la Beit el Ajaib. Saa iliyo juu ya mnara wa Beit el Ajaib ni miongoni mwa maajabu ya jumba hilo. Kila kipindi cha majira hugonga mapigo yake kuwatanabahisha wakaazi walio karibu na eneo hilo majira yao. Ingawa kwa sasa sehemu ya jumba hilo imeporomoka kutokana na uchakavu wake lakini sehemu iliyobakia pamoja na Mji Mkongwe kwa ujumla inaendelea kuwavutia watalii kutoka kona zote za dunia.

Mwaka kogwa

Sherehe ya Mwaka kogwa ni jambo la kitamaduni na imekuwa maarufu sana kule Makunduchi Zanzibar. Kwa mujibu wa historia, sherehe hizi zilianzishwa na Wapashia karne nyingi zilizopita, lengo likiwa ni kuadhimisha mwaka mpya wa Namrudh (mwanzo wa mwaka wa Kipashia). Tangu wakati huo mpaka hivi leo sherehe hizo zinadumishwa. Mwaka hadi mwaka zinapata sura mpya na kuwa kivutio kikubwa cha wanyeeji na wageni. Ufikapo katika sherehe za Mwaka kogwa utashuhudia makundi ya wageni (watalii) kutoka sehemu mbalimbali za dunia. Kwa kuzingatia ukubwa na umuhimu wa jambo hili la kitamaduni, waandishi wa riwaya wamelisawiri jambo hili kupitia kalamu zao na hivyo wamechangia kuzitangaza sherehe hizo. Waandishi hawa pamoja na wadau wengine wamechangia sana kuongezeka kwa idadi ya wageni

na watafiti wanaofuatilia sherehe hizi huko Makunduchi. Katika riwaya ya *Asali chungu*, Said Ahmed ameeleza:

Siku ya pili **sherehe za mwaka** zilianza alasiri. Ziliadhimishwa kwa ngoma za watoto wa kiume na wa kike pamoja zilizochezwa jangwani. Uwaone watoto walivyojipamba kwa kanzu na kanga mpya mpya. Nyuso zao zimepakwa podari na wanja zimejitokeza machoni. Midomo yao imerembwa rangi nyekundu na nyengine imedokezwa mashavuni kwa nakshi nzuru nzuri za viduara. Nywele zao zimesukwa kwa ustadi, zimewatoa kweli kweli kwa mitindo ya usuluti, vichocho na vijongo. Pia, nyweleni walitia vipande vya vitana vya rangi aina kwa aina. **Ngoma** hizo zilimalizika saa kumi na mbili magharibi. Hapo lilipigwa **goma** kubwa kama mbiu ya mgambo ili kunadi kuwa karamu ya mwaka tayari... (*Asali chungu*: 121).

Katika nukuu hii mwandishi anatuonesha namna sherehe ya mwaka kogwa inavyofanyika. Mwandishi anatufunulia sehemu ya sherehe na tunabaini kuwa sherehe zinatoa fursa kwa watu wa rika zote yaani watoto kwa watu wazima, wanawake kwa wanaume. Maelezo kama haya yanadokeza yanayofanyika katika sherehe na hivyo kuinua ari ya msomaji kutaka kujua zaidi. Hapa mwandishi ametoa mchango wake katika kuutangaza utalii wa kiutamaduni ambapo sherehe za Mwaka kongwa kwa Zanzibar ni sehemu muhimu ya utamaduni. Watu wengi wamekuwa wakifika na kujionea namna sherehe hizo zinavyofanyika. Kwa usimulizi huu wa mwandishi ni wazi kuwa riwaya ya Kiswahili inayo michango adhimu katika kuvifichua na kuvitangaza vivutio vya utalii Zanzibar.

Eneo la Darajani

Eneo la Darajani ni kitovu cha jiji la Zanzibar. Eneo hili limekuwa maarufu sana enzi na enzi. Ni eneo lenye mkusanyiko na mchanganyiko wa shughuli mbalimbali za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii zinazofanyika Zanzibar. Eneo hili linajumuisha soko kubwa, majengo ya kihistoria, maduka ya aina kwa aina ya bidhaa kama vile vyakula, mavazi na vifaa vya kielekroniki. Kwa mgeni afikaye Zanzibar bila kufika eneo la Darajani huwa kama kwamba hajafika Zanzibar. Kwa namna lilivyo eneo hilo huwavutia pia watalii wengi wanaotembelea Zanzibar. Kila upitapo sehemu hiyo hutakosa makundi ya wageni yakitalii katika viunga na vichocho vya Darajani. Kwa mnasaba wa harakati za eneo la Darajani, waandishi wa riwaya

nao wamechochea kulifakharisha eneo hilo. Tuone dondoo lifuatalo kutoka riwaya ya *Vuta n'kuvute*:

Kwa wana mji wa Zanzibar, **Darajani** ni pahala maarufu sana. Siku zote **Darajani** huambatanishwa na wingi wa maduka, biashara za kila aina na wingi wa magari. **Darajani** pia huambatanishwa na shughuli za kidini kama vile 'Jahusein' siku za muharram na maandamano ya dhikri yanayopitia hapo kila siku ya Ijumaa baada ya wachaMungu kumaliza kusali El Jumaa. Pia, **Darajani** ni midani ya wanasiasa wanapotaka kuhutubia mikutano ya hadhara (*Vuta n'kuvute*: 137).

Dondoo hili linadokeza kuhusu hali ya eneo la Darajani na wingi wa shughuli zake kwa Wazanzibari. Bila shaka waandishi wanalenga kupiga mbiu kwa wageni kuja na kulitembelea eneo hili ambalo linatoa sura nzima ya Zanzibar na Wazanzibari. Bila shaka bwana Shafi anao mchango kupitia dondoo hili katika kuwahamasisha wageni wa nje na wa ndani ya Tanzania kutembelea Darajani na kuchangia kwa namna moja au nyingine kustawisha uchumi wa nchi kupitia utalii.

Historia na mabaki ya kikoloni

Kama inavyofahamika, Zanzibar kama zilivyo nchi nyingine barani Afrika ilipata kutawaliwa. Vuguvugu la kudai uhuru lilipotawala katika fikra za wananchi wa Afrika, Zanzibar nayo iliingia katika sura hiyo. Kufuatia mbinyo na adha za kikoloni, Wazanzibari nao walifanya jitihada za kutafuta kujitawala. Hatimaye Zanzibar ikawa huru katika mwaka 1964. Ingawa uhuru ulipatikana, lakini bado historia na alama za kutawaliwa zipo hadi leo. Ili kulinda historia ya nchi, serikali ya Zanzibar ilianzisha Idara ya Nyaraka na Mambo ya Kale. Katika idara hiyo na sehemu nyingine kadhaa kuna nyaraka na majengo yanayoonesha historia ya tawala mbalimbali za Zanzibar. Vitu hivyo, vimekuwa vikiwavutia watalii kufika na kujioneo utajiri huu muhimu wa kihistoria. Aidha, kuna masimulizi kuhusu harakati za kudai uhuru. Masimulizi haya yanataja hali, vikwazo na shida tele walizopitia Wazanzibari katika kudai uhuru. Mwandishi Shafi Adam alionesha namna wazalendo walivyokuwa mstari wa mbele kupambana na kutafuta uhuru wa Zanzibar. Dondoo lifuatalo linafafanua zaidi:

Inspekta Wright alikuwa amekaa ofisini mwake kama mwehu, simu zinalia mtindo mmoja ikiwacha hii inalia hii na mara nyingine simu zote mbili hulika kwa pamoja akawa hajui aisikilize ipi. Alikuwa amebabaika ameinamia meza. Ameghumiwa hajui afanye nini. Simu ikalia tena.. brr brr brr.. Inspekta Wright akabakia kuitumbulia macho hajui afanye nini kwani alikuwa na hakika yatakuwa yale yale.

Akainua ule mkono wa simu taratibu kama mtu aliyechoka sana. Aliitikia kwa sauti ya mtu aliyekata tamaa.

Afande! Iliita sauti katika simu. Naongea kutoka kituo cha polisi cha Mahonda. Mahonda nzima zimebandikwa karatasi za kudai uhuru. Haijulikani nani aliyefanya kazi hiyo.

'Same old story' Inspekta Wright alilalamika. *Basi mekwisha sikia...* alijibu kisha akauweka mkono wa simu chini (*Vuta n'kuvute*: 188-189).

Data hii inaonesha wazi namna Zanzibar ilivyopita katika misukosuko ya ukoloni kama zilivyo nchi nyingine. Mwandishi anaonesha kuwa haikuwa kazi rahisi kwa wenyeji kuupigania uhuru na kumuondoa mkoloni. Mwandishi anafunua pazia na kutuonesha pia harakati za uhuru na hatimaye kupatikana kwa uhuru kamili. Maelezo haya na mengine kuhusu historia ya Zanzibar yanasisimua na yanavutia watalii wengi hasa wale wa kitafiti. Masalia ya tawala za kikoloni hivi leo imekuwa chanzo cha pato la taifa kupitia sekta ya utalii wa kihistoria.

Utamaduni wa taarab

Zanzibar ina historia ndefu ya muziki wa taarab. Inasemekana muziki huu uliingia Zanzibar kutokea Misri tangu wakati wa Usultani. Muziki huo umekuwa ukibadilika namna yake kama zilivyo tanzu nyingine za fasihi simulizi. Matamasha mbalimbali ya utamaduni hufanywa Zanzibar kila mwaka. Katika matamasha hayo taarab huwa haikosekani. Kwa kuwa taarab ni kiungo cha utamaduni wa Zanzibar, watalii wamekuwa wakivutiwa na kuhudhuria matamasha yanayojumuisha muziki huo na kuchangia pato la taifa. Taarab kama sehemu ya utamaduni imeangaliwa na waandishi wa riwaya za Zanzibar. Hapa tunamwalia Shafi katika riwaya ya *Vuta n'kuvute* ambapo ameandika yafuatayo:

Mara Denge aliyakurupusha na kusema; Jumamosi ya jana mliburudika wapi?

Unaonekana bado umechoka.

Nikwambie nini? Yasmin alianza kuhadithia kulikuwa na **taarab** hiyo hapo

Mlandege mpaka kweupe.

Wewe uliimba?

Niogope!

Nyimbo gani?

Nyingi.

Kama ipi moja kwa mfano?

Yasmin aliinama chini akijitia kuona haya (*Vuta n'Kuvute*: 87).

Dondoo hili linadokeza kuhusu muziki wa taarab kwa watu wa Zanzibar. Mwandishi anatuonesha wazi kuwa taarab ni sehemu ya burudani kwa wazawa. Pia, mwandishi anatuonesha kuwa nyimbo za taarab ni maarufu kiasi kwamba hata watu wa kawaida ambao siyo wasanii wanaweza kuziimba. Kuimbika huku kwa taarab na watu wa aina kwa aina ni ishara kuwa muziki huo unakubalika na ni sehemu ya utamaduni wa Mzanzibari. Pia, hali hii inaashiria na kukazia suala la utamaduni wa taarab Zanzibar kama sehemu ya kivutio cha utalii. Kama waandishi wengine, naye Shafi hapa amechangia kukitangaza kipengele hiki muhimu cha utamaduni kinachowavutia wageni kutoka nchi mbalimbali za dunia. Mbali na riwaya kutaja muziki huu lakini pia wizara inayohusika na mambo ya utalii imekuwa ikitumia taarab kuutangaza utalii kupitia matamasha.

Hitimisho

Makala imebainisha wazi namna riwaya za Kiswahili zilivyosaidia kuibua na kutangaza vivutio vya utalii. Ni imani ya waandishi wa makala hii kwamba riwaya nyingine na tanzu nyingine za fasihi andishi zimegusia maeneo mengine mbalimbali ya kiutalii. Hivyo, ipo haja ya uchunguzi zaidi ufanywe ili kusaidia mataifa kuvitambua vyanzo vingine vya utalii ndani ya Zanzibar, Tanzania na Afrika ya Mashariki yote kwa ujumla. Kwa upande mwingine, riwaya zote zilizotafitiwa zimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Pia, matokeo ya utafiti huu yanaonesha umuhimu mkubwa wa kuzitafsiri riwaya hizo kwa lugha ya Kiingereza na lugha nyingine za kimataifa ili kuwawezesha watu wengi zaidi kuzisoma na kuviona vivutio vilivyomo. Kwa kufanya hivyo, utalii utaweza kuimarika zaidi kwa maendeleo ya uchumi. Matokeo ya makala hii yasaidie Wizara ya Utalii Zanzibar kupanga mikakati zaidi ya kuendeleza utalii wenye tija kwa kutumia fasihi yetu.

Marejeleo

- Abdulla, M. S. (1960). *Mzimu wa watu wa kale*. East African Publishing House.
- Abdulla, M. S. (1974). *Siri ya sifuri*. East African Publishing House.
- Abdulla, M. S. (1984). *Kosa la bwana Msa*. East African Publishing House.
- Bartens, H. (2003). *Literary theory: The basics*. The Jomo Kenyatta Foundation.
- Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020
- Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Standerd Books Graphics.
- Mbatiah, M. (2016). *Riwaya ya Kiswahili: Chimbuko na Maendeleo yake*. The Jomo Kenyatta Foundation
- Mohamed, M. S. (1972). *Kiu*. Longhorn Publishers.
- Mohamed, M. S. (1976). *Nyota ya Rehema*. Oxford University Press.
- Mohammed, S. A. (1977). *Asali chungu*. Shungwaya Publishers.
- Mohammed, S. A. (1980). *Utengano*. Longmann.
- Mohammed, S. A. (1990). *Kivuli kinaishi*. Oxford University Press.
- Mohammed, S. A. (1995). *Amezidi*. Longmann
- Mohammed, S. A. (2006). *Dunia yao*. Oxford University Press.
- Mohammed, S. A. (2010). *Nyuso za mwanamke*. Oxford University Press
- Mohammed, S. A. (2014). *Kamwe si mbali tena*. Oxford University Press
- Mohammed, M. (2017). Mukumo wa Said Ahmed Mohammed katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili ndani na nje ya Afrika ya Mashariki katika Jahazi (uk. 353-367). Wakala wa Serikali wa Uchapaji.
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya uhakiki wa fasihi*. East African Educational Publishers.
- Njogu, K. & Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. The Jomo Kenyatta Foundation.
- Njogu, S. K. (1986). *Uhakiki wa riwaya za visiwani Zanzibar*. University of Nairobi.
- Njogu, S. K. (1987). *Maudhui ya mapinduzi katika riwaya za visiwani Zanzibar*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijchapishwa)
- Senkoro. F. E. M. K. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa lugha na fasihi*. Kiuttu

Shafi, A. S. (1978). *Kuli*. Tanzania Publishing House

Shafi, A S. (2001). *Vuta n'kuvute*. Tanzania Publishing House

Walibora, K. (2010). “Uhalisia na uhalisia mazingaombwe: Mshabaha kati ya dunia yao na The tin drum” katika *Swahili Forum* (uk. 17, 143-157)